

MWONGOZO WA KUSAHISHA KIDATO CHA KWANZA.

MASWALI

(a) Taja kiongozi wa kike wa Wagiriama. (AI 2)

Mekatulili wa Meddza. ✓

(b) Jamii ya Wagiriama hupatikana eneo gani hapa nchini? (AI 1)

Pwani. ✓

(c) Malalamishi ya wagiriama dhidi ya wanzungu yali husu nini? (AI 2)

- (i) Kuchukuliwa wanaume wao wenye siha ili wakapigane vita vikuu vya dunia. ✓
 - (ii) wanzungu kuwatoza kodi. ✓
Kuwafanyisha kazi za suluhu kwa ujira duni. ✓
- (d) Taja aliyekuwa mshiriki wa kiongozi wa Wagiriama. (AI 1)

Waije wa madorika. ✓

(e) Taja wanawake wanne viopngozu ambao wametoa huduma kwa jamii. (AI 4)

- (i) Margaret Thatcher - Uingereza ✓
- (ii) Indira Gandhi - India ✓
- (iii) Bi S. Johnson - Liberia ✓
- (iv) A. Merkel - Ujerumani ✓

MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 35)

(a) Taja sauti mbili ambazo ni nazali. (AI 2)

|m|, |n|, |ny|, |ng'| ✓

(b) Hizi nomino ziko katika ngeli gani. (AI 3)

- i) Uovu - U-YA ✓
- ii) Kiwavi - A-WA ✓
- iii) Raha - I-I ✓

Kamilisha methali zifuatazo. (AI 4)

- i) Mgala muwe na ..haki umpe. ✓
- ii) Mwenye kovi... usidhani kapoa. ✓

(d) Tegua vitendawili vifuatavyo. (AI 2)

- i) Mfalme katikati lakini watumishi pembeni. - Ulimi ✓
ii) Babu yangu amevalia koti la chuma. - Msumari ✓

(e) Andika sentensi hizi kwa wingi (AI 3)

i) Ulimi wako ungepona kama ungeenda kwa daktari.

✓ Ndimi zao zungepona kama wangeenda kwa madaktari.

ii) Msasi alijihami kwa uta na mshale.

✓ Wasasi walijihami kwa nyuta na mshale.

iii) Ulezi wenye aliopata ulimfaa.

✓ Malezi yanayopata yaliwafaa.

(f) Andika sentensi zifuatazo kwa udogo. (AI 4)

i) uso wa mtu Yule ulitutisha.

✓ Kijuso cha kijitu kile kinatisha.

ii) Vidole vya mtu huyo vinauma.

✓ Vijidole vya vijitu hivyo vinauma.

(g) Andika vinyume vya maneno yafuatayo. (AI 2)

i) Jenga- bomoa ✓

ii) Nasa- nasua ✓

(h) Sahihisha sentesi zifuatazo. (AI 4)

i) Mwalimu ako katika darasani. ✓ Mwalimu yuko darasani.

Mwali nguko katika darasa.

ii) Mama anapogonjeka hakulangi wali.

✓ Mama anapougua hali wali. ✓ Mama anapomwa hali wali.

i) Taja aina tatu kuu za sentensi za Kiswahili. (AI 3)

i) Sentensi Salili ✓

ii) Sentensi ambatao ✓

iii) Sentensi changamano ✓

(j) Nyambua vitenzi vifuatavyo katika kauli ulizopewa katika mabano. (AI 3)

- i) Inama (kutendesha) - inamisha ✓
- ii) Enda (kutendeshwa) - endeshwa ✓
- iii) Cheza (kutendeana) - chezeana ✓

(k) Tunga sentensi mbili kuonyesha matumizi ya alama ya koloni/nukta pacha. (AI 2)

(l) Onyesha miundo ya maneno yafuatayo. (Alama 2)

i) Nchi- KK I ✓

ii) Imba- I K K I ✓

(m) Eleza maana ya nomino. (AI 1)

Ni nero kinalotunika kutajia kitu au mtu. ✓

4. ISIMUJAMII (AI 10)

(a) Lugha ni nini? (AI 1)

Ni mfumo wa sauti nasibu unaotuniwa na binadamu kuwasiliana. ✓

(b) Taja sifa tano za Lugha (AI 5)

- ✓ Lugha ina uwezo wa kukua kwa msamiati wake kupanuka.
 - ✓ Lugha ina uwezo wa kufa kwa msamiati wake kupotea.
 - ✓ Lugha zote ni sawa. Hakuwa bora kuliko nyingine.
 - ✓ Kila lugha ina sauti zake maalum.
 - ✓ Lugha tubadilika kutegemea mazingira na mapito kwa wakati.
 - ✓ Lugha hutofautisha binadamu na mnyama.
 - ✓ Lugha ina uwezo wa kuunganisha au kutenganisha.
- (c) Eleza maana ya; Jamii kutegemea matumizi yake.

- ✓ i) Lafudhi- upekee wa mtu kimatamshi.
tofauti kimatamshi kwa warungumzaji wa lugha moja.
- ✓ ii) Sajili/rejesta- Ni matumizi ya lugha katika muktadha fulani wa Jamii.
- ✓ iii) Lahaja- Namna mbalimbali za kurungumza lugha moja kuu.
- ✓ iv) Isimu- sayansi ya lugha.

Kuondhesha
Kuandika tarehe.
Kuadika saa.

5. FASIHI SIMULIZI (AI 20)

(a) Eleza maana ya fasihi. (AI 2)

✓ Ni Sanaa inayotumia lugha kuchamkua vipengele mbalimbali vya maisha ya binadamu.

(b) Taja dhima tano za fasihi. (AI 10)

- ✓ Huburudisha jamii
- ✓ Huelelisha jamii
- ✓ Hukuza uwero wa kufikiiri.
- ✓ Hukuza maadili.
- ✓ Hukuza ulianii na ufasaha wa lugha.
- ✓ Huonya na kushauri.
- ✓ Huelekeza.
- ✓ Huendeleza utamaduni wa jamii (zozote tano)

(c) Taja sifa nne za mtambaji wa hadithi. (AI 8)

- ✓ Mwenye ujasiri wa kuzungumza hadharani.
- ✓ Awe na ufahamu mpana wa lugha.
- ✓ Awe na uchangamfu na ncheshi.
- ✓ Awe na uwero wa ufaraguzi.
- ✓ Awe na uwero wa kushirikisha hadhira yake.
- ✓ Awe na kumbukumbu nzuri
- ✓ Aweze kubalisha toni au kiimbo.
- ✓ Aweze kuwa na ufasaha na ujuzi wa lugha.
- ✓ Awe na uwero wa kutumia ishara za uso, mwili na miondoko.
- ✓ Aweze kuelefahamu utamaduni wa hadhira yake.

(zozote nne $4 \times 2 = 8$)